ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake

38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
53.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
55.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
57.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
58. Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini

59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
62.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
63.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
65.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
66.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
67.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
68.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
69.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
72.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani

79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndg Yahya Khamis Hamad	**Kny: Katibu wa Baraza la Wawalishi**

Kikao cha Nane – Tarehe 27 Januari, 2012

Kikao kiliaza saa 3:00 asubuhi

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 46

Hatma ya Waathirika wa *MV Spice Islanders*

Mhe. Hamza Hassan Juma – Aliuliza:-

Katika ajali ya meli iliyozama ya *MV SPICE ISLANDER* kuna Watanzania wengi hasa Wazanzibari waliopoteza ndugu na jamaa zao pamoja na mali zao, na kuna baadhi ya familia wamebaki watoto tu, wazazi wao wote wamepotea katika ajali hiyo.

a) Je, ni hatua gani serikali yetu itachukua kuwahudumia mayatima walipoteza wazazi wao katika ajali hiyo.

b) Je, hadi sasa kuna mpango gani wa kuwaangalia wajane walioachiwa ulezi na waume zao waliofariki au kupotea katika ajali hiyo.

c) Je, serikali yetu imejifunza kitu gani kutokana na uzembe uliosababisha tukio la ajali hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hmza Hassan Juma swali lake Nam. 46 lenye vifungu a, b na c kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikiwahudumia watoto yatima ambao wamekosa huduma hizo kutoka kwa jamaa zao kupitia vituo vya kulelea watoto yatima ambavyo vipo tokea baada ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964. Hata hivyo, serikali baada ya kupokea ripoti ya Tume iliyoundwa ya Kuchunguza Ajali ya *MV Spice Islander 1* tayari imeyafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa na tume hiyo. Hatua za kisheria na kinidhamu zinaendelea kuchukuliwa ili kila mhusika apate haki zake kwa mujibu wa sheria.

Aidha, fedha ambazo zimechangwa na wananchi na wahisani mbali mbali watapatiwa wananchi walionusurika katika ajali hiyo na wale waliofariki mgao wao watapatiwa warithi wao kwa kufuata utaratibu maalum ili kila mmoja apate haki yake.

Mhe. Spika, jambo la kujifunza katika ajali hii ni suala zima la kuheshimu sheria na taratibu ziliopo pamoja na uwajibikaji na kila mhusika kufanya wajibu wake kwa mujibu wa sheria na taratibu ziliopo. Pia kuhakikisha sheria inachukua mkondo wake kwa wale wote watakaoshindwa kusimamia au kutimiza majukumu yao.

Hata hivyo, napenda kutoa wito kwa wananchi nao kuheshimu sheria na taratibu zilizopo na kutoa taarifa kwa mamlaka husika pale sheria na taratibu hizo zinapopindwa ama kuvunjwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa lakini vile vile niishukuru Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kazi nzuri iliyofanywa na Tume aliyoiteuwa Mhe. Rais kwa ajili ya masuala ya *MV. Spice Islander*.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri alivyojibu swali langu la msingi swali la (a) alilijibu kijumla jumla namna ya kuwahudumia watoto yatima, lakini swali langu zaidi lilikuwa linagusa maalum kwa hawa mayatima ambao wazazi wao wamepatwa na ajali ya *MV. Spice Islander*. Kwa kuwa hawa mayatima hivi sasa wapo na wanahudumiwa na ujamaa zao na wengine wanaowahudumia ni watu ambao uwezo wao mdogo.

Je, haoni kwamba baada ya kuwa ripoti imeshakamilika na tayari kuna baadhi ya fedha zilizochangwa, sasa hivi muda umefika kuharakisha kuhakikisha kwamba wanatathmini hawa mayatima na kuanza kuwashughulikia.

Lakini pili, katika swali la (c) nilipouliza niliuliza serikali inajifunza kitu gani kutokana na uzembe uliosababisha tukio hili. Jawabu la Mhe. Waziri amesema atajaribu kuangalia kuhakikisha kwamba watu wanatekeleza nidhamu katika utendaji wa kazi.

Sasa swali langu je, hatuoni kwamba serikali kuwa na muhali sana hasa kuwashughulikia wale ambao wanafanya makosa mbali mbali yakasababisha ajali ndio inayosababisha kuendelea kutokea haya matukio mara kwa mara.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii kupokea shukurani alizozitoa kwa serikali kwa kuipongeza kuchukua hatua ambazo zinatokana na mapendekezo ya tume iliyoundwa ya kuchunguza ajali ya meli hiyo.

Mhe. Spika, mayatima hawa ni watoto wetu na tunao utamaduni katika familia zetu kwa ndugu na jamaa kulea mayatima hawa. Lakini kama nilivyosema katika swali langu la msingi serikali tokea baada ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 imekuwa na utaratibu wa kuwalea mayatima wale ambao hawana ndugu na jamaa wa kuwashughulikia. Kwa hivyo, utaratibu huo upo na kwa

wale wote ambao walipata ajali katika *MV Spice Islander 1* na jamaa na ndugu zao wakashindwa kuwalea watoto hao basi serikali siku zote itakuwa tayari kuwasaidia watoto hao kwa kupelekwa katika vituo vya kulelea watoto yatima.

Mhe. Spika, kwa kuwa katika utaratibu huo pia wa fedha ambao zimechangwa kwa ajili ya kusaidia waliohusika na ajali ile, taratibu sasa zimekamilika na ni hivi karibuni tu serikali itatoa utaratibu wa namna ya mgao ule, tutahakikisha wale wahusika wote wamefanikiwa wakiwemo wale wajane ambao watalea mayatima hawa ama wazee wengine wote wale watakaolea mayatima hawa. Kwa sababu wale wote waliokuwemo katika ajali ile mgao wao utagawiwa kwa kila mmoja wao.

Kwa hivyo, nataka nilihakikishie Baraza lako tukufu wale waliofariki warithi wao kwa utaratibu maalum watakabidhiwa fedha hizo na wale walionusurika katika ajali vile vile watapata mgao wao.

Kuhusu muhali. Mhe. Spika, serikali inafanya kazi kwa mujibu wa Katiba na Sheria zilizopo. Hivyo, tutachukua kila hatua kuhakikisha kwamba sheria zinafuatwa na muhali unaondolewa ili wale wote watakaotenda makosa basi wawajibike kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Mhe. SAleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na mimi nichukue fursa hii kuipongeza serikali kwa kuweza kuandaa utaratibu ambao uko njiani kukamilika ili hizo fedha zilizopatikana kuweza kupelekwa kwa walengwa.

Mhe. Spika, kwa kuwa kuna taarifa kwamba baadhi ya watendaji wetu katika ngazi za chini huko mawilayani, katika shehia, uaminifu wao ni mdogo sana. Je, ni utaratibu gani ambao

utatumika ili fedha hizi serikali kuu kuhakikisha kwamba zimewafika walengwa na sio kupenya hapo kati kati.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nipokee pongezi alizozitoa kwa serikali. Mhe. Spika, utaatibu tuliokusudia kuufanya ni kuishirikisha Serikali Kuu, masheha pamoja na Wakuu wa Wilaya. Kwa sababu zoezi hili tulishawahi kulifanya wakati wa kutoa kifuta machozi kwa wafiwa, nina hakika tutahakikisha tunachukua kila hadhari kuona kwamba makosa hayatokei.

Naelewa mawazo ya Mhe. Saleh Nassor na ni kweli wako watu ambao si waaminifu na hivi sasa wamejipanga na ndio ambao wenye maneno mengi kwa ajili ya kutafuta njia ya kula fedha hizi. Lakini yeyote yule afisa wa serikali ama mwananchi yeyote atakayefanya kushiriki katika kutoa taarifa za uongo ili apate fedha hizi, adhabu kali aingojee juu yake na malipo ya fedha hizo atayafanya.

Nam. 107

Huduma kwa Walioanguka Mikarafuu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

(a) Je, serikali ina mpango gani wa kuondoa tatizo la ukosefu wa vitanda maalum kwa watu waliovunjika uti wa mgongo kutokana na kuanguka kwenye mikarafuu.

(b) Ni wavunaji wangapi wa karafuu ambao walianguka katika mwaka huu tangu msimu kuanza.

(c) Miaka ya nyuma watu walikuwa wakianguka kwenye mikarafuu wakuliwa wakipewa fomu maalum ambazo hujazwa na daktari wa kuonyesha athari za mwili kwa

majeruhi ambazo hutumika katika tathmini ya fidia. Kwa nini watu walioanguka msimu huu hawapewi fomu hizo na badala yake hupewa fomu ya polisi ya matibabu (PF3) pekee.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 107 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Kwanza Mhe. Spika, sina budi kumpongeza Mhe. Mwakilishi kwa kufahamu umuhimu wa vitanda maalum kwa ajili ya watu wanaovunjika migongo, na kwa suala hili hasa wanaotokana na kuanguka kwenye mikarafuu.

(a) Mhe. Spika, ni imani ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwamba, Wizara ya Afya nayo inafahamu tatizo la ukosefu wa vitanda maalum kwa wanaovunjika mgongo. Kama nilivyosema kwa mantiki ya suala hili wale wanaoanguka kwenye mikarafuu.

(b) Mhe. Spika, tangu msimu huu wa karafuu ulipoanza ni wavunaji 113 ndio walioanguka mikarafuu na kutoka Mikoa yote ya Kisiwa cha Pemba kama ifuatavyo:-

Wilaya ya Mkoani watu 68, Wilaya ya Wete watu 25, Wilaya ya Chake Chake watu 17 na Wilaya ya Micheweni watu watatu (3). Mmoja kati ya watu hao Mhe. Spika, amefariki dunia.

(c) Mhe. Spika, ni kweli kwamba mwaka huu walioanguka mikarafuu hawakupewa fomu maalum za

kujaza ambazo zinaonyesha athari za maumivu kama miaka ya nyuma na badala yake wamepewa fomu za *PF3* kwa ajili ya matibabu.

Kama nilivyosema katika majibu yangu yaliyopita, hii ilitokana zaidi na kwamba *ZSTC* kupitia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ilikuwa hailipi fidia kutokana na matatizo ya kibiashara yaliyoikumba shirika hilo na hasa biashara ya karafuu siku za nyuma. Serikali itaangalia utaratibu gani mzuri wa kulipa fidia kwa wanaoanguka mikarafuu katika mageuzi mazima yanayotarajiwa kufanywa ndani ya Shirika la *ZSTC*.

Mhe. Spika, aidha, serikali inaanzisha Mfuko Maalum wa Maendeleo ya Karafuu (*Cloves Development Fund*) ambapo mfuko huo utakuwa unasaidia maendeleo pamoja na matatizo mbali mbali ya zao la karafuu kwa njia ya kuweka iwe bora zaidi na hasa kuwasaidia wakulima wa mikarafuu na pale watakapokuwa kwa bahati mbaya wanaanguka kutoka kwenye mikarafuu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kwanza nipokee pongezi zake kwa unyenyekevu mkubwa Mhe. Naibu Waziri. Kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Muyuni naomba kuuliza maswali matatu ya nyongeza.

Mhe. Spika: Kwa mujibu wa Kanuni unaruhusika kuuliza maswalia mawili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Sawa Mhe. Spika. Je, serikali itatumia utaratibu gani wa kulipa fidia ikiwa watu walioanguka kwenye mikarafuu hawakujaza fomu za athari za kuonesha kuumia kimwili. Pili, kwa kuwa vitanda vya wagonjwa waliovunjika uti wa mgongo ni muhimu katika masuala ya tiba.

Serikali ina mpango gani wa dharura wa kununua vitanda hivyo kabla msimu ujao kuanza.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kama mtu hakujaza fomu ya *PF3* sirahisi kwa serikali kuhakikisha kwamba kweli huyu ameanguka kwenye mkarafuu. Na kwa hivyo, kupitia kwako Mhe. Spika, niwahamasishe Waheshimiwa Wawakilishi kuwaambia wananchi umuhimu wa kujaza fomu hizi ili kuwa ni kithibitisho kwamba kweli watu hawa wameanguka kwenye mikarafuu.

Lakini suala zima la fidia Mhe. Spika, kama nilivyosema wakati najibu maswali mbali mbali kwamba tuna mpango mzima wa kufanya *restructuring* ya *ZSTC* pamoja na mpango wa serikali pia wa kuanzisha mfuko huu wa kuendeleza zao la karafuu. Basi katika utaratibu huo suala hili pia litazingatiwa la kuwapa fidia wale ambao wanaanguka kutoka kwenye mikarafuu. Lakini Mhe. Spika, suala la umuhimu wa vitanda vya watu wanaovunjika mgongo nimesema kwenye jibu langu la awali kwamba suala hili ni imani yangu kuwa Wizara ya Afya inalitambua na bila shaka italipa umuhimu wake.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri nina swali la nyongeza. Mkoa wa Kusini Pemba ni mkoa unaoongoza kwa uzalishaji wa zao la karafuu na takwimu za watu walioanguka Wilaya ya Chake Chake na Mkoani ni watu 85 ni sawa na asilimia 75.2 ya watu walioanguka. Kwa kuwa karafuu mara hii zimepatikana zaidi ya tani 4000. Je, serikali itachukua motisha gani kwa wale walioanguka kutengewa fungu maalum ili nguvu na ari ya kupanda mikarafuu na kuchuma ziweze kuongezeka kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, nimetangulia kusema na tunaendelea kusema kwamba

serikali inatambua umuhimu wa kuwashughulikia hao wanaoanguka katika mikarafuu na ndio maana tumesema suala hili litazingatiwa kwa kina zaidi hapo tutakapoanzisha Mfuko wa Kuendeleza Zao la Karafuu.

Mhe. Spika, Mfuko huu tunategemea kwa kiasi kikubwa kwamba utalizingatia kwa undani suala hili kuona kwamba ni kiasi gani basi pesa zitakazopatikana kutokana na kuendeleza Mfuko huu wa Karafuu zilengwe kwenye kuwashughulikia wagonjwa watakaoanguka kutokana na kuanguka kwenye mikarafuu.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi tuwe na subira, tusubiri mpango huu mzuri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwani nayo inalifahamu tatizo hili na ndio maana Mhe. Rais alipoongeza bei ya kununulia karafuu kutoka kwa wakulima ikaelekeza kwamba, asilimia 80 ya pesa zile ziende kwa wakulima ili waweze na wao kwa kiasi Fulani kushughulikia suala hili. Mhe. Spika, asilimia 20 tu ndio inayobakia ndani ya Shirila la *ZSTC*.

Nam. 60

Matengenezo ya Barabara za Ndani

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman - Aliuliza:-

Baadhi ya barabara za ndani (*Feeder Roads*) zinahitaji matengenezo ili
kuwaondoshea usumbufu wananchi hususan katika Miji ya Chake-Chake na
Mkoani Pemba.

Je, Mhe. Waziri amejipangaje katika kuzifanyia matengenezo japo ya dharura barabara ya Misufini Chake-Chake kuanzia Benki ya *Barclays* kupitia Soko la Matunda Chake kwenda Hospitali ya Chake-Chake, kuelekea Soko la Samaki hadi kiwanja cha Mpira

Tibirinzi, barabara ya Miembeni Chake-Chake hadi Afrikana, na barabara kuanzia soko la zamani Mkoani hadi Skuli ya Ng'ombeni. Pia barabara ya kuanzia Msikiti wa Ijumaa Mkoani kupitia Mikarafuuni Kinyasini hadi kufikia Ofisi ya Mwani Mkoani.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 60 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba baadhi ya barabara za ndani (*feeder Roads*) zinahitaji matengenezo ili kuwaondoshea usumbufu wananchi wetu katika shughuli nzima za usafiri.

Aidha, katika kuwaondoshea usumbufu wa usafiri katika maeneo Mbale mbali, wizara yangu kupitia Idara ye Ujenzi na Utunzaji Barabara na kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara imepanga na imepania kwa kuifanyia matengenezo ya kuipandishia lami barabara ya Misufini, Chake-Chake kwa kuanzia Benki ya *Barclays* kupitia soko la matunda Chake-Chake kwenda Hospitali ya Chake na mwishoni hadi uwanja wa mpira wa Tibirinzi. Mhe. Spika, kazi hii tuna matarajio kwamba itafanyika katika robo ya tatu ya bajeti ya mwaka 2011 – 2012.

Mhe. Spika, kuhusu barabara nyengine wizara yangu itazifanyia ukaguzi wa kina ili iweze kuzitafutia njia bora ya utekelezaji wake katika bajeti yetu ya mwaka 2012 – 2013.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na kwamba swali la msingi la Mhe. Shadya

Mohammed lilikuwa kuhusu barabara ya Mikarafuuni na Tibirinzi, lakini Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali la msingi alieleza kwamba wizara imo katika mchakato wa kuziangalia barabara mbali mbali ambazo ni *feeder roads* ambazo zinataka kusaidiwa.
Je, Mhe. Spika, katika hizo barabara nyengine za *feeder roads* zilizokuwa hali mbaya sana zinazotaka kufanyiwa tathmini. Je, barabara yangu ya Kwa Abass Husein/Shaurimoyo hadi Mboriborini na Daraja bovu imo. Pili, kama imo kwa kuwa ahadi ya Mhe. Waziri katika kikao cha Bajeti aliniahidi kwamba angelinifanyia ukarabati wa dharura angalau kile kipande kidogo kinachotoka kwa Abass Hussein mpaka juu kwa Sheha wa Shehia ya Shaurimoyo.

Tatu, katika wizara yake kuna fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya Wizara yenyewe ya Mawasiliano na Utunzaji wa Barabara lakini pia Mfuko wa Barabara. Je, hizi fedha za Mfuko wa Barabara wanazitumia katika utaratibu gani ili zisiingiliane zika *overlap* ile bajeti ya Wizara ya Mawasiliano.

Mhe. Spika: Hii inaitwa kupora swali chini ya mwavuli wa *feede roads***,** lakini kimsingi maswali yalikuwa yanahusu miji ya Chake Chake na Mkoani Pemba, ndio swali la msingi. Lakini chini ya mwavuli wa *feeder roads* sijui utasaidiaje Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, katika maelezo yetu wakati tunajibu jibu mama suala lililoulizwa ni barabara ya Tibirinzi na kilichoulizwa ni barabara za *feeder roads*. Katika swali hili kulikuwa kuna zaidi ya hiyo barabara moja ambayo Mhe. Mwakilishi alitaka kupata majibu yake.

Lakini zaidi nilichokieleza hapa ni kwamba, mpango wa wizara yetu tunatambua kwamba Unguja na Pemba ina *feeder roads* nyingi ambazo zinahitaji kufanyiwa ukarabati na kauli hiyo

tunaendelea kuisisitiza kuwa, barabara hizi za mijini zinapaswa kutengenezwa na kusimamiwa na Halmashauri na Manispaa. Lakini kwa kuliona hilo wizara yetu tumekuwa na utaratibu wa kushirikiana na Halmashauri hizo na Manispaa katika kufanya ukarabati.
Aidha, nakubaliana na Mhe. Hamza kwamba wizara yetu iliahidi kumtengenezea barabara hiyo katika bajeti inayofuata mwakani na niseme tu kwamba, kilio chake cha kufanyiwa ukarabari wa barabara ya Kwa Abas Hussein – Sheha wa shehia ya Shaurimoyo tumekisikia tutawatuma wataalamu wetu wakaangalie na tutaona kwa kushirikiana na wenzetu wa Mfuko wa Barabara kama kuna uwezo wa kasma wanaweza kutusaidia tunaweza tukamsaidia Mhe. Mwakilishi.

Vile vile kuhusiana na fedha zinazotumika ni kwamba fedha tunazoziomba hapa ni zile za miradi mikubwa ndizo ambazo tunasimamia sisi wizara moja kwa moja na fedha za ukarabati wa barabara ndogo ndogo tunapata kwa kupitia wenzetu wa Mfuko wa Barabara.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba atashirikiana na Halmashauri na Manispaa katika kurekebisha *feeder roads*, lakini katika Manispaa ya Zanzibar atakumbuka kwamba walipopewa mamlaka ya kutengeneza njia za ndani pia walipewa mamlaka ya kukusanya kodi za *road license* pamoja na ***leaner.*** Kwa bahati mbaya au nzuri kodi hizo zimeondoshwa na zimepelekwa Serikali Kuu.

Je, haoni kuendelea kuipa mamlaka Manispaa ni kuibebesha mzigo waliokuwa hawauwezi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, tunachokizungumza hapa ni wajibu wa taasisi zetu kama serikali, wajibu wa Manispaa ni kutunza miji ikiwemo pia

kurahisisha njia za kutumizi pamoja na usafi. Mhe. Spika, tulichokieleza wizara yetu kwa kushirikiana na Manispaa katika ujenzi, masuala ya kodi, tunaamini kwamba pamoja na kuwa fedha hizo zinakusanywa na serikali lakini bado Manispaa ina vyanzo vya kutosha vya kuweza kuendeleza miradi hii.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa mji wa Chake Chake mara nyingi barabara zake zikiharibika zinachukua muda mrefu kutengenezwa na vyombo hivi viwili ndio vyenye usimamizi. Wajibu wa Baraza la Manispaa au Mabaraza ya Miji ni kushughulikia lakini usalama wa wapitanjia na vyombo vya usafiri ni juu ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Je, Mhe. Waziri haoni kwamba ipo haja sasa ya kufanya mkakati wa dharura wa kuangalia kwamba hizi barabara zinatengenezwa mapema iwezekanavyo kabla haijasababisha ajali au madhara mengine kwa wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, tumeeleza katika majibu mama kwamba mpango wa wizara yetu kuzifanyia ukarabati barabara hizo za Chake Chake ni katika robo ya tatu ya mwaka huu wa fedha 2011/2012. Matumaini yetu kwamba hivi sasa tuna matatizo ya mitambo, tukiweza kutengeneza mitambo yetu tutajitahidi kwamba *material* iliyopo ya lami, mafuta na fedha ambazo zimetengwa kuweza kufidia ili kuweza kunusuru barabara hizi zisiathirike zaidi.

Nam. 62

Ujenzi wa Daraja la Mto Zingwe Zingwe

Mhe. Mlinde Mabrouk Juma - Aliuliza:-

Mheshimiwa Rais wa Zanzibar alipokuwa katika kampeni zake katika Jimbo la Bumbwini miongoni mwa mambo aliyoyaahidi ni ujenzi wa daraja la mto Zingwe Zingwe.

Je, Mhe. Waziri ni sababu zipi zilizopelekea kutotimizwa kwa ahadi hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 62 kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, napenda kukubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba Mhe. Rais wa Zanzíbar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati alipokuwa katika kampeni zake katika Jimbo la Bumbwini miongoni mwa mambo aliyoahidi ni ujenzi wa daraja la Mto Zingwe Zingwe. Wizara yangu imeipokea ahadi hiyo na imejipangia kuitekeleza katika bajeti ya 2012 – 2013 kupitia fedha za mfuko wa barabara.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mafupi lakini mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Rais alipokuwa katika kampeni mbali ya daraja hilo la Zingwe Zingwe yapo madaraja ambayo aliahidi atayafanyia kazi kwa ajili ya kuleta ustawi wa barabara zetu likiwemo daraja la Chuo cha Amali Mkokotoni.

Mhe. Spika, daraja hili lilijengwa kwa nguvu na ari mpya kwa haraka sana lakini hatimae lilianguka bila ya kuarifiwa Wazanzibari. Naomba kujua daraja hili lilianguka kwa nini na gharama gani ziliingia daraja hili. Baada ya kujengwa hivi sasa limeonekana halikujaa sawa sawa na usawa wa barabara. Je, ni kwanini kiufundi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ni kweli kwamba eneo la Mkokotoni karibu na Chuo cha Amali kulikuwa kuna daraja ambalo limevunjwa na limejengwa daraja jipya ikiwa miongoni mwa miradi ya madaraja manne ikiambatana na lile la Mwera, Maji mekundu na Mto mchanga.

Mhe. Spika, napenda kumthibitishia Mhe. Mwakilishi kwamba ujenzi uliojengwa pale umezingatia vigezo, ni ujenzi mzuri na una uthibitisho kwamba anachokiona pale sio kuwa *level* ya daraja lile haliko sawa sawa, ujazo ule umezingatia na kina cha maji ya mto ule yatakapoweza kujaa ili kuweza ku-*flow* vizuri.

Nam. 99

Ofisi ya Ustawi wa Jamii Pemba

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Inasemekana kwamba Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto haina jengo la ofisi huko Pemba na badala yake imekuwa ikikodi majengo mbali mbali kwa ajili ya kuendesha shughuli zake.

(a) Je, Mhe. Waziri, taarifa hizo ni kweli.
(b) Kama ni kweli huoni kwamba kuendelea kukodi majengo kwa ajili ya wizara hiyo huko Pemba ni mzigo kwa serikali.
(c) Wizara ina mpango gani wa kulipatia ufumbuzi suala hilo.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 99 lenye vifungu a, b na c kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto haina jengo la ofisi Pemba.

(b) Wizara imelazimika kukodi jengo moja tu na sio majengo mbali mbali kwa muda ili kukidhi mahitaji na kuziwezesha ofisi zake kutekeleza majukumu yake ya kila siku ya kuwahudumia wananchi bila ya usumbufu.

(c) Mhe. Spika, kuhusu suala la kukodi jengo la ofisi kuwa ni mzigo kwa serikali nakubaliana nae kwa upande mmoja kwamba serikali inalazimika kumlipa mwenye nyumba kodi yake kwa mujibu wa mkataba. Lakini kwa upande mwengine jambo hili si mzigo kwa vile serikali imekodi jengo ili kuziwezesha taasisi zake kutoa huduma kwa jamii zinazohitajika ambazo thamani yake ni kubwa kuliko kodi ya jengo. Serikali imelazimika kukodi jengo kwa muda na kwa dharura baada ya ofisi yetu ya Pemba kuwa na ufinyu wa nafasi za kufanyia kazi kwa ufanisi kama nilivyoeleza hapo juu.

(d) Mhe. Spika, Wizara ama Serikali kwa ujumla ina mpango wa kujenga majengo yake yenyewe kwa ajili ya ofisi Unguja na Pemba mara tu uwezo ukiruhusu ili kuondokana na tatizo la kukodi majengo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, serikali imekuwa ikitumia kiasi gani kwa mwaka kulipa gharama za kodi ya nyumba na utaratibu gani unatumika katika kutafuta jengo la kupanga.

Mhe. Spika, swali (b) kwa vile serikali imesema ina mpango wa kujenga jengo Unguja na Pemba. Je, mradi huo unatarajiwa kuanza mwaka gani ili kuokoa fedha za umma kutumika kukodi majengo ya watu binafsi.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwanza naomba nimwambie kwamba sisi tumekodi lile jengo kwa muda wa mwaka mmoja na tumefunga nae mkataba mwenye nyumba kama kawaida ya kiserikali.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu mama kwamba mara tu serikali itakapokuwa tayari basi hakuna haja ya kupoteza pesa za serikali tutahama tutarudisha lile jengo kwa sababu hali ya jengo lililokuwepo zamani ambalo wizara kwa kule Pemba wakikaa kufanyia kazi kwa kweli lilikuwa ni finyu sana. Kwa hivyo, ikiwa tayari serikali tutahama maana lazima tufanye namna ya kupata mapesa kidogo.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na kuwa ofisi hiyo kutokuwa na jengo Pemba lakini pia kumekuwa na malalamiko kwamba Kitengo cha Ustawi wa Jamii kutokufanya kazi zake hasa kuwasaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu na badala yake kazi hiyo hufanywa na *NGOs* kama WAMATA Chake Chake.

(a) Je, Mhe. Waziri ana kauli gani juu ya malalamiko haya.
(b) Kama Wizara ina mpango gani wa kulichukulia hatua suala hili.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwanza mimi nilikuwa sina habari kwamba kuna malalamiko hayo.

Mhe. Spika, jibu (b) Kitengo cha Ustawi wa Jamii kinafanya kazi zake Pemba kama kawaida. Ufinyu wa majengo kweli tunao lakini wizara kama tunavyofanya kazi hapa Unguja na Pemba inafanya kazi vile vile.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa wizara hii si mpya ni wizara iliyokuwepo zamani sana.

(a) Kabla ya kuhamia katika jengo hili walilokodi je, jengo hilo wizara walilokuwa wakifanyia kazi lilikuwa ni jengo la serikali au binafsi.

(b) Kama lilikuwa ni jengo la serikali na sasa wameamua kuhamia jengo la kukodi la binafsi. Je, hawaoni kwamba wangebakia katika ofisi yao ile ile na zile fedha wanazokodia wakajengea nyumba ambayo itakuwa ni ya serika,

(c) Kwa sababu wizara hii ni ya zamani je, kuna sababu ipi ya msingi mpaka leo hii kuwa hata wizara haina jengo lake.

(d)

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, ni kweli wizara hii ni ya zamani si ya jana na leo lakini tangu hapo zamani ilikuwa kwa Pemba hatuna ofisi tulikuwa tunajibanza katika ofisi za serikali ambapo tulikuwa hatulipi kodi.

Kwa kipindi hichi mpaka ikafikia kuwa tukodi nyumba kwa kweli hali ya kazi zimeongezeka watu walikuwa wanafanya kazi kwa shida sana na ndio maana ikabidi tuhamie katika jengo lile. Serikali yenyewe iliridhika kuona kwamba wafanyakazi wetu

pamoja na wale wanaokwenda kwa kuhudumiwa wanapata shida ndio maana ikabidi tukodi hapa.

Lakini huko nyuma kote tulikuwa tunakaa katika majengo ya serikali.

Nam. 109

Fungu la Bodi ya Mikopo Zanzibar

Mhe. Mohammed Said Mohammed – Aliuliza:-

(a) Katika mwaka wa fedha 2012/2013 serikali imejiandaa vipi katika kuongeza fungu la Bodi ya Mikopo Zanzibar ambalo katika mwaka wa 2011/2012 lilitengewa fedha zisizotosha kukidhi mahitaji ya waombaji wa mikopo hiyo.

(b) Je, serikali imejiandaaje kuondoa tofauti ya kielimu baina ya wenye uwez na wasio na uwezo.

(c) Je, serikali imejiandaaje kuondoa tofauti ya kijinsia na tofauti ya maeneo baina ya mjini na vijijini katika kuwapatia elimu ya juu wananchi wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 109 lenye sehemu a, b na c kama hivi ifuatavyo:

(a) Mchakato wa kuandaa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2012/2013 hivi sasa umeanza na wizara yangu inakusudia kupendekeza kuongezwa kwa ruzuku iliyotolewa kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa na kuweza kutoa mikopo kwa waombaji wengi zaidi.

Katika Bajeti ya mwaka 2012/2013 bodi imeomba jumla ya Tshs. 7.3 bilioni.

(b) Kati ya hizo Tshs. 4.0 bilioni ni kwa ajili ya wanafunzi wanaoendelea na masomo na zilizobakia ni kuwakopesha wanafunzi wapya. Kwa vile mchakato wa kuandaa Bajeti ya mwaka 2012/2013 ndio kwanza umeanza, ni mapema mno kuweza kujua Bodi ya Mikopo itatengewa kiasi gani.

(c) Tokea mwaka 1964 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikitekeleza Sera ya Elimu bila ya malipo kwa nia ya kuondoa tofauti za kielimu baina ya wananchi wenye uwezo na wasio na uwezo. Sera hiyo imefanikiwa sana kufikisha huduma za elimu maeneo yote nchini kwetu mjini na vijijini.

(d) Mkakati wa kuondoa tofauti za kijinsia na tofauti za maeneo baina ya mjini na vijijini katika utoaji wa elimu ya juu umekuwa ukitekelezwa. Mkakati huo unatekelezwa kuanzia ngazi ya msingi na sekondari kwa kuhakikisha kuwa skuli nzuri zinaenezwa katika sehemu zote za nchi yetu ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wa vijijini wanapata huduma nzuri za kielimu sawa na wanafunzi wa mjini.

Kwa msingi huo, Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Skuli za Sekondari unaotekelezwa kwa pamoja na Benki ya Dunia na Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika *(BADEA)*, unajenga skuli 21 ambazo zimeenea katika wilaya zote za Unguja na Pemba. Mradi huu utaongeza sana kuwa na skuli nyingi na za kisasa katika sehemu za vijijini.

Kwa upande wa wanafunzi wa kike, hivi sasa asilimia ya wanafunzi wa kike katika elimu ya maandalizi, msingi na sekondari ni kubwa ukilinganisha na asilimia ya wanafunzi wa kiume. Hali hiyo ya ongezeko la asilimia ya wanafunzi wa kike imesaidia sana katika kuongezeka kwa idadi na asilimia ya wanafunzi wa kike wanaoendelea na masomo ya elimu ya juu.

Kwa mfano, katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar wanafunzi wa kike wanaosomea shahada na stashahada mbali mbali ni asilimia 52 na wanaume ni asilimia 48. Kwa jumla katika vyuo vikuu vilivyopo Zanzibar asilimia ya wanafunzi wa kike ni zaidi ya asilimia 45 ya wanafunzi wote. Hii ni wazi kuwa tofauti ya kijinsia katika upatikanaji wa elimu ya juu imepungua sana. Vile vile wanafunzi wanaojiunga na vyuo vikuu wanatoka katika maeneo yote ya nchi yetu mijini na vijijini.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana na marefu ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza niipongeze sana wizara yake kwa kuongeza zaidi ya asilimia 90 ya bajeti hii hapo mwakani. Lakini vile vile tulikuwa mwaka jana tuna bajeti ya Tshs. bilioni 4 safari hii tumeongeza Tshs. bilioni 3. Je, Mhe. Waziri hahisi kwamba wizara yake pesa zilizoongezwa hazikidhi haja kwa wanafunzi wapya ambao wataingia mwakani.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli ongezeko la pesa ambalo tumeliomba katika bajeti yetu linaweza likawa halikidhi haja. Kwa mfano, mwaka huu ambao tunakwenda nao tulikuwa na wakopaji 1603 ambao walikuwa wanahitaji Tshs. Bilioni 15.3 ili waweze kuendelea na masomo yao.

Lakini Mhe. Spika, niseme kwamba tunashona kanzu kwa mujibu wa kitambaa tulichonacho. Bodi ya Mikopo wenyewe tumewapa mamlaka ya kutafuta pesa pahala popote ikiwa kwa mikopo, ruzuku au msaada na tayari Bodi ya Mikopo imeandaa utaratibu wa kuwasiliana na mabenki yetu, wafanyabiashara ili kuhakikisha mfuko wetu huu unatuna na kuweza kukidhi haja ya wanafunzi wetu ambao wanaomba.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, ni sababu zipi zinazosababisha wizara yake Mhe. Waziri kutotoa mikopo kwa wanafunzi ambao wanaomba mkopo kwa kwenda kusoma nchi za nje.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kikawaida Bodi yetu ya Mikopo huwa inatoa nafasi kwa wanafunzi kwenda kusoma nje, lakini kwa mwaka huu haikuweza kutoa nafasi kwa wanafunzi wetu kwenda kusoma nje. Ni kweli kama kuna wanafunzi karibu 201 ambao waliomba kwenda kusoma nje lakini kutokana na ambavyo nimeeleza hapa katika jibu langu la msingi kwamba tulikuwa na tatizo la bajeti. Mhe. Spika, wanafunzi ambao waliomba ni 1603, tuliomudu kuwapa ni kama wanafunzi 191 tu. Kwa hivyo, hapa naomba Mhe. Mwakilishi aone ni tatizo gani tulilokuwa nalo.

Jengine Mhe. Spika, hili naomba niwashauri waombaji wetu ambao wanaomba katika Bodi ya Mikopo. Kwa zile fani ambazo zinapatikana ndani ya nchi basi ni vizuri waombe kwa kupitia vyuo vya ndani ya nchi.

Kwa mfano, Mhe. Spika, kumsomesha daktari nje ya nchi kwa miaka mitano au sita tunahitaji karibu Tshs. 70 milioni, lakini kuna vyuo kwa mfano kama vya Muhimbili daktari huyo huyo tunaweza kumsomesha kwa Tshs. 25 milioni na si zaidi ya hapo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuuliza swali moja dogo sana la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa tangu zamani, sasa na baadae Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ipo na itaendelea kuwepo. Kwa kuwa sasa serikali ya SMZ haizungumzii tena siasa za mivutano inazungumzia maendeleo. Kwa kuwa taifa lolote haliwezi kuendelea bila ya wataalam.

Je, ni lini SMZ itakatisha mambo ya kutumia mafedha mengi kwa ajili ya sherehe na kuzisukuma fedha hizi katika kutoa elimu ili serikali yetu iendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kweli muasisi leo kanishangaza kidogo, yeye ndio wa mwanzo hapa kutaka sherehe zetu za Mapinduzi ziwe kubwa na kwa vyovyote vile zitahitaji fedha katika kuzifanya sherehe ziwe kubwa na nzuri. Kwa hivyo, leo muasisi kidogo kaenda kinyume na maneno yake ya kawaida.

Mhe. Spika, sherehe tunazozifanya ni kwa nia ya kuweka kielelezo na historia ya nchi yetu na kukumbuka siku ya taifa letu na si kwa nia ya kuharibu fedha za umma. Ni wajibu wetu kufikiria watoto wetu wanaosoma ili nao wapate fedha kwa ajili ya kuwasomesha watoto wetu.

Mhe. Spika, wazo la kupunguza matumizi katika suala zima la sherehe serikali inalifanyia kazi ili fedha tunazozipata zitumike katika shughuli zetu za maendeleo.

Nam. 127

Wanafunzi wa Sekta ya Afya

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza**:-**

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa muda mrefu imekuwa ikichukua hatua za kuongeza wataalamu katika sekta ya Afya kupitia vyuo vyake.

(a) Inakuwaje wanafunzi wanaosoma katika vyuo hivyo hawalipwi posho zao za kujikimu kwa muda muafaka.

(b) Wizara ya Afya kwa muda mrefu wanafunzi wapatao 12 ambao wakilipwa posho ya 80,000/= kwa mwezi ni sababu gani wanafunzi hao wameshindwa kupata posho zao kwa zaidi ya miezi mitatu na kuwafanya wasome katika mazingira magumu.

(c) Kwa kuzingatia Chuo cha Afya *Zanzibar Medical School* kwa upande wa Pemba kwa nini wanafunzi wake hawapewi huduma ya usafiri kama ilivyo kwa wanafunzi wa Unguja.

Mhe. Waziri wa Afya - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 127 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:

(a) + (b) *Zanzibar Medical School* ni kimoja kati ya vyuo vya Wizara ya Afya ambacho kiko chini ya kifungu cha bajeti ya miradi ya maendeleo ya Wizara na kinapata fedha zake kutoka Serikalini. Ili Wizara iweze kuwalipa inategemea upatikanaji wa fungu hilo. Katika maombi ya kila mwezi fedha za posho la wanafuzi hao huombwa kwa utaratibu uliowekwa na fungu likiingiziwa fedha basi hulipwa. Ni kweli kwa kipindi cha miézi mitatu kutokana na upungufu wa fedha katika serikali kuu kifungu hicho hakikupata fedha lakini mwezi ulioingiziwa wanafunzi walilipwa pamoja na

malipo ya malimbikizo yao. Baada ya hapo sasa wanapata fedha hizo kwa kawaida.

(c) Tawi la *Zanzibar Medical School* liliopo Pemba, lina gari ambalo limeharibika na kipuri chake hakipatikana nchini. Utaratibu umefanywa kwa kuazimwa gari ya mpango wa kudhibiti kichocho na ndilo linalotumika kuwasafirisha wanafunzi. Lakini sio kweli kwamba wanafunzi wa Unguja nao wana gari. Wao wakihitaji usafiri wanakodiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali langu moja lenye vifungu (a), (b), (c) na (d). Mhe. Naibu Waziri je, wizara yako ina mpango gani wa kuondoa tatizo hilo la posho

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, hebu maswali hayo yawe mafupi kidogo. Maana swali (a),(b),(c) na (d), nadhani hayana mtiririko. Lakini yawe ni mafupi tena ni mawili tu ya nyongeza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika.

(a) Je wizara yake Mhe. Naibu Waziri ina mpango gani wa kuondoa tatizo hilo la posho lisijitokeze katika siku za baadae, ili kuwaondoshea usumbufu na kuwavunja moyo wanafunzi hao.

(b) Wizara ya Afya mwaka jana ilipeleka wauguzi kisiwani Pemba ili kuondoa upungufu kwa wauguzi, sababu gani zilizopelekea wauguzi hao kuanza kuondoka Pemba kwa kasi kubwa na kusababisha usumbufu kwa wagonjwa wanaohitaji msaada maalum hasa kwenye matumizi ya dawa, kuzingatia ratiba. Mfano hospitali ya Chake-Chake, kuna tatizo la upungufu wa wauguzi.

(c) Kamati katika kazi zake imebaini kuwa hakuna gari la kuazima iliyotolewa
kwa wanafunzi hao. Hadi kamati inamaliza kazi zake kisiwani Pemba, je utakuwa tayari kushirikiana na kamati hiyo kuionesha gari hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, swali (b) halina uhusiano na swali hili, hilo sitojibu.

Mhe. Spika, tumepanga utaratibu wa wanafunzi kuwepo Unguja na wanafunzi kuwepo Pemba. Kundi la mwanzo lipo Unguja na kundi la pili lipo Pemba na watakaofuata tutawapanga kwa utaratibu huo huo. Hii inafanyika ili nao kujaribu kupunguza upungufu wa wafanyakazi waliopo kule, kwa sababu wanafunzi wakiwe kule nao wanafanya shughuli zao katika hospitali, wanajifunza na wakati huo huo wanasaidia upungufu wa wafanyakazi. Kwa hivyo, utaratibu huo utaendelea. Kama gari itakuwa mbovu kama ilivyo hivi sasa, hivyo vitengo ambavyo ndio tunakoazima gari navyo ni vya Wizara ya Afya. Kwa hivyo, tunajitahidi wanatupa na tunajitahidi kuwatilia mafuta, hivyo wanafunzi huwa hawapati usumbufu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu ambayo sikuyapenda ya Mhe. Naibu Waziri, naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kwanza naomba nikumbushe kwamba mwenye wajibu wa kukataa swali ni Spika, sio waziri au naibu waziri. Mhe. Spika, ninachopenda kumuuliza ni kwamba wanafunzi wa *Zanzibar Medical School* waliopo Pemba, ambao ni 12 wengine wanatoka Tumbatu na Makunduchi.

(a) Je, unapompeleka mwanafunzi Pemba bila ya kulipa posho la zaidi ya miezi mitatu, wizara yako inakusudia apate wapi huduma za maisha.

(b) Unaliambia Baraza kwamba Pemba mnaazima gari na Unguja hamna gari mliyowakodia wanafunzi. Je, unakusudia kuniambia kwamba taarifa ambazo wizara yako imeipatia kamati tangu mwaka jana ni za uongo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ningeomba arudie swali la pili. Swali la kwanza nimelifahamu. Lakini swali la pili sijalifahamu.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, rudia swali.

Mhe. Hija Hassan Hija: Swali la (b) Mhe. Spika, ni kwamba Mhe. Naibu Waziri amesema kuwa wanafunziwa Pemba wanakodiwa gari au wanaazimiwa gari, jambo ambalo sina hakika nalo kama ni kweli. Lakini pia Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba Unguja hawajawahi kukodiwa gari.

Napenda kumuuliza kwamba taarifa ambazo wajumbe wa kamati hii ya ustawi wa jamii wanapewa tangu mwaka jana, wizara yake inakusudia kutuambia kwamba ni taarifa za upotoshaji na sio za kweli.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya:

(a) Mhe. Spika, kama nilivyosema katika jibu mama, kuwa Chuo cha *Zanzibar Medical School* kiko katika mpango wa maendeleo wa serikali, tunaweza kuwalipa tu posho kama tutapewa, kama hatukupewa hatuna cha kuwalipa. Lakini hilo ni posho haina maana kwamba wale wanafunzi wanaishi kwa kutegemea posho la Shs. 80,000/=. Wale ni wanafunzi wana makwao na wazee wao wanawasaidia. Posho huwa inatolewa pale inapopatikana na sasa hivi wanapewa.

Mhe. Spika, kwa ile miezi mitatu nakubali hilo ni kweli hawakupewa, lakini zilipopatikana walipewa na mpaka sasa hivi wanapewa.

(b) Mhe. Spika, kuhusu suala la gari

UTARATIBU

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, kanuni ya 58(3), naomba Mhe. Spika, kwa heshima kubwa na taadhima ya hali ya juu uniruhusu nikinukuu ambacho kinasema kwamba;

Kifungu cha 58(3)

> "Mjumbe yeyote anapokuwa anasema Barazani atawajibika kuwa na sababu za msingi kwamba maelezo anayoyatoa ni sahihi na sio mambo ya kubuni au ya kubahatisha tu".

Mhe. Spika, hili suala la kwamba kila mwanafunzi aliyeko katika hiki chuo cha *Medical School* kuwa wana makwao.

Naomba Mhe. Naibu Waziri afute usemi wake kwa sababu, katika darasa liliopo Pemba la wanafunzi 12, karibu wanafunzi 6 ni kutoka Unguja tena katika maeneo ya Tumbatu, Nungwi na kadhalika, sasa wale wanafunzi hawana makwao. Kwa hivyo, hapa Mhe. Naibu Waziri anakiuka ibara ya 58(3), kwa heshima kubwa naomba afute maneno yake.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa ruhusa ya kuongeza maelezo ya Mhe. Naibu Waziri wangu. Mhe. Hija Hassan alisema mwenyewe kwamba wanafunzi walioko Pemba wengine wanatoka Unguja. Mhe. Naibu Waziri wangu hakukataa hilo. Kwa hivyo, anapoambiwa kasema uongo ni kuongeza chumvi vile vile.

Mhe. Naibu Waziri wangu alichosema ni kwamba wanafunzi wanapopewa Shs.80,000/= hata sisi tunaamini kwamba mwanafunzi hawezi kuishi kwa Shs. 80,000/= Pemba, isipokuwa ni posho linalowasaidia matumizi madogo madogo na wakati huo ilivyokuwa pesa hazijapatikana, na zilipopatikana basi walilipwa zote pamoja na *area* na sasa tatizo hilo la kutokulipwa halipo. Tunaomba Waheshimiwa Wajumbe wafahamu hivyo, wasilazimishe ilivyokuwa sivyo tunavyoeleza. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Saleh Nassor Juma, tatizo liko wapi kwani.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, nadhani Mhe. Waziri hili jibu limetolewa sasa hivi na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza wamo. Alisema Mhe Naibu Waziri kwamba wanafunzi wanaosoma katika *Medical School* wako majumbani kwao, sasa hivi kasema. Mimi ndio nikajenga hoja kwa kupitia ibara hii ndio nikatoa maelekezo ya kanuni, kwamba maneno haya sio ya kweli. Kwa sababu mimi niko katika kamati ya maendeleo ya wanawake na ustawi wa jamii, nimepata maelezo ya wanafunzi wenyewe kwamba wengine wanatoka Tumbatu na Nungwi na wanasoma katika *Medical School* iliyoko Pemba. Kwa hivyo, maneno haya sio ya ukweli na naomba yasiingie katika kumbukumbu za Baraza, kwa sababu itakuwa Mhe. Naibu Waziri kalipotosha Baraza, kwa hivyo yafutwe.

Mhe. Spika: Kiini cha tatizo bado sijakipata, ili niweze kutoa muongozo. Kile kiini cha tatizo liko wapi bado sijakipata. Hebu kuwa muwazi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, kiini cha tatizo ni kwamba Mhe. Naibu Waziri tunaomba akubali kuwa, hawa wanafunzi walioko katika *Medical School* kule Pemba, wengine wanasoma wakiwa ugenini hawako majumbani kwao, wana shida za usafiri na makazi vile vile hawako kwao.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri, anachosema Mhe. Saleh Nassor Juma ni kwamba wanafunzi walioko kule Pemba wengine hawako makwao, kwa sababu wanatoka maeneo mbali mbali kutoka huku Unguja. Sasa hebu kama hilo uliteleza kidogo liangalie namna ya kusawazisha usemi huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba nikufahamishe nilichokisema na ninataka anifahamu. Wanafunzi wa *Medical School* walioko Unguja na walioko Pemba wote wengine wanatoka Pemba na wengine wanatoka Unguja. Kwa hivyo, walioko Unguja nusu wanatoka Pemba na nusu wanatoka Unguja na walioko Pemba nusu wanatoka Unguja na nusu wanatoka Pemba.

Kwa hivyo, nilichokisema ni kwamba wanachopewa ni posho, hao wanafunzi posho ya Shs. 80,000/= ni kuwasaidia, lakini wao wana makwao. Mhe. Spika, ina maana akiwa anakaa Pemba na Tumbatu ni kwao na wazee wao wanawasaidia na serikali inawasaidia posho, ndicho nilichosema.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nafikiri tofauti ilikuwa ni kufahamu. Wana makwao kwa maana wana wazee wao wanaweza kuwasaidia, licha ya kwamba atakuwa yuko Pemba, lakini huku Unguja wazee wanawasaidia ndio iliyokuwa maana yake. Sio kwamba ni kwao kule Pemba wakati ni mtu wa Tumbatu.

Kwa hivyo, nadhani hapo hakuna tofauti ni tatizo la ufahamu. Hata hiyo maana unayoisema inaweza ikawa, lakini maana yake ilikuwa ni hiyo. Tuendelee.

Nam. 48

Jumba la Kulelea Watoto Forodhani

Mhe. Hamza Hassan Juma – Aliuliza:-

Mhe. Waziri, siku ya ufunguzi wa Bustani ya Forodhani, aliyekuwa Rais wa Zanzibar Dk. Amani Abeid Karume aliahidi kuwa ataagiza wizara yako kulifanyia matengenezo jengo la watoto mayatima hapo Forodhani kuwa ni Museum for Maritime for East African ambapo makumbusho hayo yangeliweza kusaidia kuitangaza Zanzibar kwa kuzidi kuwavutia watalii na watafiti ili kuongeza ajira na mapato kwa nchi yetu.

(a) Mhe. Waziri, Je, taarifa hiyo unayo.
(b) Kama wizara yako inayo taarifa hiyo, Je, mmechukua juhudi gain kulitekeleza suala hilo.
(c) Je, wizara yako inawaambia nini wananchi kuhusu jengo hilo la watoto yatima hapo Forodhani

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 48 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, wizara yangu haina taarifa kwamba kuna agizo la kulifanyia matengenezo jengo la watoto mayatima lililoko Forodhani.

(b) Mhe. Spika, tunalolifahamu sisi ni kuwa suala la matengenezo ya jengo hilo liko mikononi mwa Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe, inayosubiri jibu kutoka Jumuiya ya Aghakhan iwapo bado ina nia ya kulifanyia jengo hilo liwe ni Indian Ocean, ili Mji Mkongwe uendelee na matengenezo.

(c) Mhe. Spika, wizara yangu inachoweza kuwaambia wananchi ni kwamba jengo hilo lilikuwa ni la watoto mayatima haliko katika mkono wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, naomba nimuulize swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Spika, kwa utaratibu Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anapokwenda katika shughuli yoyote huwa ana ambatana na mawaziri, baadhi ya makatibu wakuu, wakurugenzi na watendaji mbali mbali wa serikali.

Kwa bahati nzuri, siku ya uzinduzi wa Bustani ya Forodhani hata na mimi mwenyewe nilikuwepo siku hiyo, na Mhe. Rais Mstaafu wa Zanzibar alitoa maelekezo baada ya kuwa na *rumors* nyingi kuhusu jengo lile la Forodhani na alitoa maelekezo kwamba jengo lile liwekwe kama museum au kama makumbusho, litengenezwe liwe makumbusho kwa ajili ya wale mabaharia na ile historia ya mabaharia kwa nchi za Afrika ya Mashariki.

Sasa Mhe. Waziri anaponiambia leo kwamba hakumbuki na naamini katika serikali hii Mhe. Spika, iliyochaguliwa tena, asilimia karibu 70 bado ni watendaji wale wale wa serikali. Sasa suala hili Mhe. Spika, mimi nataka nimuulize hapa

(a) Je, baada ya kupata suala langu, alijaribu kuwasiliana na Ofisi ya Rais Ikulu ili kupata taarifa kuhusu suala hili.

(b) Alisema kwamba wao wanasubiri Aghakhan Foundation ambao wako tayari kwa ajili ya kuboresha eneo lile. Wizara wakati Mhe. Waziri aliposema kwamba Aghakhan wao walikuwa ndio waendeleze

jengo hili. Je, waliwahi kuwafuata Jumuiya ya Aghakhan wakawauliza hatua waliyofikia.

(c) Mhe. Spika, kwa kuwa bado agizo la Mhe. Rais Mstaafu wa Zanzibar, tunaliona ni jambo la maana na la msingi lingeweza kusaidia kuongeza idadi ya watalii na historia kwa ajili ya Zanzibar. Je, wizara kuanzia leo itachukua hatua gani ili kuhakikisha kwamba jengo lile linashughulikiwa kama maagizo ya Rais Mstaafu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alivyoagiza.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa ufupi ni kwamba kama Mhe. Naibu Waziri wangu alivyojibu kwenye jibu mama ni kwamba lile jengo haliko mikononi mwetu.

Haidhuru Mhe. Rais Mstaafu alitoa agizo hilo, lakini bado hatujakabidhiwa hilo jengo. Sio hilo tu, hata lile jengo la Forodhani la Peoples Palece, wajenzi hasa wanaohusiana na ujenzi wa majengo ni Mamlaka ya Mji Mkongwe, sio sisi, pamoja na kwamba sisi ni dhamana wa mambo ya makumbusho.

Mhe. Spika, swali lake jengine la kwamba kama tumeshaanza mawasiliano na Aghakhan. Mhe. Spika, hatuwezi kufanya mawasiliano na Aghakhan kwa sababu mkataba wetu sio sisi na Aghakhan, ni mkataba wa Mji Mkongwe na Aghakhan, sisi hatuna mawasiliano kabisa na Aghakhan.

Mhe. Spika, pia sio vibaya kwamba lile jengo tupewe sisi, kwa sababu ni masuala ya historia na ni moja katika sera yetu.

Basi tutalichukua hilo wazo na tutalifuatilia vipi, ili tuweze kukabidhiwa lile jengo liwe mikononi mwetu tuweze kuendesha shughuli za kiutalii. Lakini mpaka sasa jengo haliko ndani ya

mikono yetu, pamoja na kwamba Mhe. Rais Mstaafu alitoa agizo hilo, bado hatujakabidhiwa.

Kwa hivyo, maagizo yale ilikuwa ni wao Mji Mkongwe watukabidhi sisi, lakini bado. Ahsante sana.

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena, kama nilivyosema jana kwamba ninasikitika sana hasa katika utendaji wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Spika, tunapozungumza suala na tunapopeleka sisi katika wizara

Mhe. Spika: Kuhusu utaratibu kuna kanuni iliyokosewa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: kwa sababu katika *collective responsibility* kama waziri, Mhe. Spika, tunapopeleka suala tukaambiwa halihusiani na wizara yetu. Mhe. Spika, bado kuna tatizo. Hata jana Mhe. Spika, nilieleza, suala tunapopeleka katika wizara, kama wenyewe wanahisi sio la kwao, basi walirejeshe Baraza la Wawakilishi na watowe maelekezo lipelekwe katika wizara husika.

Mhe. Spika, lakini mimi maswali yangu nimeuliza zaidi ya miezi mitatu nyuma. Sasa tunapoambiwa halihusiani na wizara hii, Mhe. Spika, bado tuna tatizo, inaonesha ndio pale mawaziri, ina maana kila moja anafanyakazi na ofisi yake, hawafanyikazi kwa pamoja. Mhe. Spika, tunataka kauli za serikali ziwe zinafanana.

Kwa hivyo, mimi naomba Mhe. Spika, hili ni kosa la pili kwa wizara hii ya habari, naomba sana Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, anapoona swali kapelekewa halihusiani na wizara yake basi alipeleke katika wizara husika au

alirejeshe Baraza la Wawakilishi, ili lipelekwe pahala panapohusika. Vinginevyo Mhe. Spika, kuna maswali mengine yanapochukua muda mrefu sana basi mambo mengi yanakuwa yanaharibika.

Mhe. Spika: Hiyo ni sawa. Lakini kwa upande mwengine serikali ndio iko hapa. Kama kuna waziri ambaye anajua taarifa ya jambo hilo juu ya swali hili hili basi anaweza akanyanyuka waziri mwengine akaweza kusaidia majibu, ni utaratibu wa kawaida.

Sasa kama hakuna basi nadhani swali hili lingetayarishwa vizuri ili tukapata majibu yaliyokuwa mazuri. Lakini ni utaratibu wa kawaida. Kuna baadhi ya maswali yanagusa wizara hii na nyengine na nyengine. Sasa inapotokezea kwamba sehemu ya swali lile limegusa wizara nyengine, basi ni utaratibu waziri anayeguswa pale yeye huwa anajibu. Tumeona mara nyingi hata Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, anajibu maswali ya mazingira lakini limeulizwa pengine kwenye utalii. Sasa yeye anaingia pale kusawazisha swali lile, hivyo ni utaratibu wa kawaida. Kwa hivyo, inaonekana hakuna majibu zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kutoa ufafanuzi wa ziada kuhusu jambo ambalo liko mbele yetu. Mhe. Spika, ni kweli kwamba serikali inafanya kazi kwa pamoja na ni wajibu wa waziri muhusika pale ambapo swali limekuja, ikiwa halihusiani na wizara yake awasiliane na wizara husika.

Mhe. Spika, kwa sababu jambo hili linahusu Mji Mkongwe na waziri muhusika hayupo sasa hivi. Kwa hivyo, naomba Baraza lako liendelee na majibu yatatolewa katika kikao kitakachokuja cha Baraza hili lako tukufu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja hiyo.

Mhe. Spika: Kwa sababu hoja hii ya majengo, hata sisi tulikuwa tuna jengo moja pale Baraza la Wawakilishi la zamani, jengo lile halikukabidhiwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Lilikaa muda mrefu likawa linayumba yumba. Nadhani hivi karibuni tu ndio ukatoka uamuzi.

Sasa kama na hili lilikuwa limeagizwa likabidhishwe kwa wizara hii, nadhani utaratibu ungefanyika ili likawa lina mwenyewe sasa wa kuliangalia. Vyenginevyo linaweza likaharibika bure. Nafikiri tuendelee. Lakini utaratibu huu wa kama swali halihusiani na wizara ni kweli, lirejeshwe ofisini ili lipelekwe kwenye wizara inayohusika mapema iwezekanavyo. Tuendelee.

Nam. 98

Ujenzi wa Kituo cha One Stop Center Chake-Chake

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Kuna taarifa kwamba wizara inayohusika na masuala ya ustawi wa jamii imeomba gofu linalotumiwa na hifadhi ya mambo ya kale Chake-Chake Pemba kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha *One Stop Center* katika eneo hilo.

(a) Je, Mhe. Waziri, taarifa hizo unazo.

(b) Kama unazo huoni kwamba ni vyema kuwapatia gofu hilo kwa ajili ya ujenzi huo kwa vile kituo hicho ni muhimu kwa jamii hivi sasa.

(c) Ni lini gofu hilo litakabidhiwa kwa Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 98 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, idara ya makumbusho na mambo ya kale halijapokea rasmi ombi la ujenzi wa kituo cha *One Stop Center* katika eneo la gofu la Chake Chake Pemba.

(b) Mhe. Spika, gofu hilo ni eneo la kihistoria na limetangazwa rasmi mwaka 1986. gofu hilo liko chini ya dhamana ya Idara ya Makumbusho kwa mujibu wa sheria ya uhifadhi ya mwaka 2000.

(c) Mhe. Spika, idara ina mpango wa kuyatanua makumbusho hayo kwa ajili ya shughuli zake za kiidara.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri katika jibu lake amesema kwamba hajapokea taarifa, lakini mimi naanza kumtangulizia taarifa. Kwa sababu najua kamati ilipokuwa ikifanyakazi hiyo taarifa imeshapelekwa, labda iko njiani kama tulivyozowea, tuko njiani au tuko mbioni.

(a) Mhe. Spika, naomba Mhe. Naibu Waziri atumie nafasi hii ili kutueleza ni kipi muhimu katika matumizi ya jengo hilo, kati ya makumbusho ya mambo ya kale na uanzishwaji wa kituo hicho cha *One Stop Center*.

(b) Je, Mhe. Waziri utachukua hatua gani za kunufaikisha upatikanaji wa gofu hilo, hasa ukizingatia tatizo la unyanyasaji wa watoto Zanzibar ni tatizo la taifa na

kila wizara na taasisi ina wajibu wa kupiga vita vitendo hivi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante Mhe. Spika. Mhe. Mjumbe ameuliza kipi ni muhimu kati ya *One Stop Center* na Makumbusho ya Mambo ya Kale.

Mhe. Spika, labda mimi niseme tu kwamba yote ni muhimu, kwa sababu kila mmoja amekabidhiwa dhamana yake, madamu amekabidhiwa dhamana yake basi ni muhimu. *One Stop Center* ina umuhimu na Makumbusho ya Mambo ya Kale vile vile ina umuhimu.

Mhe. Spika, kama Mhe. Naibu Waziri wangu alivyojibu katika swali mama, kwamba hatujapata barua rasmi ya ombi hilo. Lakini wakiomba ni suala la kulitizama, si tutazungumza tu. Lakini bado hatujapata agizo rasmi kwamba bwana, tunahitaji hili jengo kwa ajili ya jambo fulani. Mhe. Spika, naomba kidogo arudie lile swali jengine.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika. Swali langu jengine ni kwamba Je, wizara itachukua hatua gani za kunufaikisha upatikanaji wa gofu hilo, hasa kwa kuzingatia tatizo la unyanyasaji wa watoto Zanzibar, ni tatizo la kitaifa na kila wizara au taasisi na viongozi tuna wajibu wa kupiga vita vitendo hivi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante Mhe. Spika. Hatua tunazochukua labda ni kuzungumza na wenzetu wanaotaka kuanzisha kituo hicho cha *One Stop Center*, nini hasa lengo na tunajali sana. Yaani tunajali kuhusiana na masuala ya unyanyasaji wa watoto ni masuala yetu kwa pamoja na sote tunajali, sio kwamba hatujali.

Hapana, lakini kwa sababu taratibu lazima zifuatwe. Lile ni jengo letu na wao wanalihitaji basi wajibu ni kutuomba, watuandikie barua tu basi halafu tutakaa tutazungumza. Ni hilo tu Mhe. Spika, ahsante.

Katibu wa Baraza la Wawakilishi: Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwamba sasa tumefikia mwisho wa shughuli za Baraza lako kwa mujibu wa orodha wa shughuli za leo. Pia Mhe. Spika, hapa ndio tumefikia mwisho wa shughuli zilizopangwa kwa ajili ya Mkutano wa huu wa Sita wa Baraza la Nane la Wawakilishi la Zanzibar.

Naomba kutoa taarifa Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla hatujaendelea na sehemu ya shughuli yetu iliyobaki, naomba nitowe maelezo mawili au matatu.

Moja, ni kwamba Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo anawaarifu Waheshimiwa Wajumbe Wanawake, kwamba yale mazoezi yao wanayofanya ya mpira wa *netball* yatakuwa yanaendelea kwa siku ya Jumatano, Alhamis na Ijumaa saa 12:00 za asubuhi, wapi nafikiri wanaelewa wenyewe.

Pili, Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa ameleta wageni hapa, ambao kwa bahati mbaya ilikuwa hatukuwahi pale mapema, wageni hao waliofika hapa kuja kuona shughuli zetu ni ndugu yetu Bwana Mensoria Bagwan Mshamba na mwanawe Sunnee Mensoria Bagwan Mshamba. Karibuni sana *(Makofi).*

Halafu jana kulikuwa na taarifa kidogo ambayo aliitoa Mhe. Ali Mzee Ali, juu ya kazi yao wakati huo kama Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Meli kuhusiana na taarifa ya masuala ya meli zenye matatizo mbali mbali. Waheshimiwa Wajumbe, suala ambalo walishauri katika bodi kwamba ni vyema ingepatikana meli mpya.

Sasa taatifa hii ilionekana kuwa Mhe. Omar Ali Shehe labda kidogo alitoa taarifa ambayo haikuwa sahihi.

Waheshimiwa Wajumbe, nimeletewa *hansard* hapa ambayo inahusiana na eneo hilo ambalo Mhe. Omar Ali Shehe amelieleza inasema kama hivi ifuatavyo:-

“Mhe. Spika, tulikwenda Shirika la Meli chini ya uongozi wa *Professor* kwa hapa *Professor* ni Mhe. Ali Mzee Ali, hiki ni cheo cha juu cha kisomo ambacho tulimpa sisi wenyewe ndani ya Baraza kipindi kilichopita. Chini ya uongozi wa *Professor* kama Mwenyekiti wa Bodi wa Shirika la Meli Alhajj mzee wetu Mhe. Ali Mzee Ali, basi shirika limefanya juhudi kubwa ya kutafuta meli mpya, tena ya kisasa ya abiria na mizigo na yenye kwenda kwa kasi walitafuta nchini Afrika ya Kusini kule na tayari wameshakubaliwa kila kitu”. *(Makofi)*

Sasa jambo hili Mhe. Waziri amelitolewa maelezo mazuri kama ninakumbuka vizuri, alieleza kwamba meli hiyo ya Afrika ya Kusini bei yake ilikuwa ni kubwa sana, yaani bei ya meli hiyo pengine ingeweza kununua meli kama mbili. Kwa hivyo, serikali wakaona jambo hilo halikuwa sahihi kuingia kwenye mkataba wa kuchukua chombo ambacho bei ni kubwa wakati pengine ingeongeweza kidogo basi ingewezekana kupatikana kwa meli mbili.

Waheshimiwa Wajumbe, nadhani alichokuwa akikizungumza Mhe. Omar Ali Shehe ni kile ambacho Mhe. Ali Mzee Ali alitaka kutoa taarifa. Lakini hakukuwa na tatizo na jibu lilitoka vizuri na kwa kweli yote tuliyapokea jana kwenye ripoti ile, yaani hata hilo ambalo Mhe. Waziri alijibu lilionekana kuna usahihi kwamba si vyema kwenda kununua chombo cha ghali sana, wakati fedha hizo zingeweza kununua chombo zaidi ya kimoja ambacho kifanye kazi ile ambayo ilikusudiwa. Kwa kweli hiyo ilikuwa

sababu kwa nini tusiende kwenye makubaliano ya kununua meli hii kwa njia ya mkopo. Kwa hivyo, nilitaka nitoe taarifa hiyo na inaonekana kwa taarifa hii, hili jambo limeshakaa vizuri. Nilitaka niseme hayo.

Waheshimiwa Wajumbe, nichukue nafasi hii kuwashukuru katika mkutano huu, ambao ulikuwa na miswada miwili tu, lakini mambo mengine mengi yamejitokeza na yote kimsingi tuliyafanyiakazi kwa kadri ya hali ilivyokuwa pamoja na mazingira. Kwa kweli mashirikiano makubwa ya kuendesha kikao hiki yamefikia hapo kwa msaada mkubwa ambao Mhe. Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wawili wamenipa katika kuongoza Baraza hili. Vile vile kwa mashirikiano makubwa sana ya Waheshimiwa Wajumbe wote pamoja na Mawaziri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, shughuli hizi zisingeweza kwenda vizuri kama si kwa msaada mkubwa sana, ambao makatibu wetu hapa walikuwa wanafanya hiyo kazi, ili kuona shughuli zetu zinakwenda kama tulivyozipanga. *(Makofi)*

Pamoja na hayo, waandishi wetu wa habari walijitahidi kutoa taarifa hizi, ingawa baadhi ya wakati zilikuwa zinatatiza kidogo. Lakini kimsingi wananchi walikuwa wanapata habari ya nini kinachoendelea hapa katika Baraza lao.

Kwa hivyo, nichukue nafasi hii kuwapongeza wote walioshiriki kwa namna moja au nyengine katika shughuli zetu za Baraza na kufanikisha kumaliza mkutano wetu huu. *(Makofi)*

Baada ya hayo, sasa nimuombe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, karibu. *(Makofi)*

KUAHIRISHA KIKAO

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nianze kwa

kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kuendelea kuijaalia nchi yetu kuendelea na amani na utulivu na kutuwezesha kukutana na kufanikisha Mkutano huu wa Sita wa Baraza la Wawakilishi.

Pia naomba kuchukua fursa hii, kukushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kuliendesha Baraza letu kwa mafaniko makubwa. Kama kawaida yako umeendelea kuwa mfano mzuri wa kuwa na busara, uadilifu na hekima kubwa katika kuliendesha Baraza letu.
Mhe. Spika, natoa shukrani za pekee kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa uongozi wake uliojaa busara na hekima na unaozingatia maslahi ya wananchi. Mhe. Dkt. Shein ameendelea kuwa mfano bora wa uongozi makini, ambao sote tunatakiwa kuiga mfano huo katika nafasi zetu mbali mbali, ili nchi yetu iendelee kupata heshima na maendeleo ya haraka. *(Makofi)*

Agizo la Mhe. Rais wetu la kututaka tubadilike sisi wenyewe pamoja na watendaji wetu, ni lazima sasa tulifanyie kazi kwa vitendo na hapo ndipo tutakuwa tunamsaidia Mhe. Rais wetu kutimiza azma na malengo yake ya kuiletea nchi yetu maendeleo.

Mhe. Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa umakini wao wa kuhoji, ili kupata ufafanuzi wa masuala mbali mbali yaliyowasilishwa katika Baraza lako Tukufu. Kuuliza maswali na kutoa maoni yao kwa uwazi wakati wa kujadili Miswada iliyowasilishwa hapa Barazani. Naamini kwamba kufanya hivyo ni kwa lengo la kuimarisha demokrasia na utendaji mzuri wa shughuli za serikali na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, vile vile, nawashukuru kwa dhati Waheshimiwa Mawaziri kama ilivyo kawaida yao kuendelea kutoa ufafanuzi wa hoja za Wajumbe na kujibu maswali yote 127 pamoja na yanyongeza kwa makini, ufasaha na usahihi. *(Makofi)*

Aidha, usikivu na utulivu waliouonesha wakati wanapopata hoja za Wajumbe na kukubali kupokea ushauri, kunadhihirisha ukomavu wao kwenye uongozi katika kipindi hiki cha kuzidi kuimarika kwa demokrasia katika nchi yetu. Ni matumaini yangu kwamba wananchi waliokuwa wakifuatilia kwa karibu zaidi mijadala ya kikao hiki, wamefaidika na majibu na ufafanuzi uliotolewa na Waheshimiwa Mawaziri. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika Mkutano huu wa Sita Baraza lako limepokea na kujadili Miswaada miwili ya Sheria ambayo ni:-

(i) Mswaada wa Kufuta Sheria ya Ulipaji wa Mafao ya Viongozi wa Kitaifa Nambari 4 ya Mwaka 1988 na Sheria ya Viongozi wa Kisiasa Nambari 6 ya Mwaka 1999 na Kutunga Sheria Mpya ya Maslahi na Mafao ya Viongozi wa Kisiasa Baada ya Kustaafu Pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

(ii) Mswada wa Sheria ya Kuanzishwa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, Kazi zake, Uwezo wake na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, vile vile katika Kikao hiki Baraza lako limeweza kupokea na kujadili Hoja ya Jambo la Dharura iliyowasilishwa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu kuhusiana na hatua ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwasilisha maombi kwenye Umoja wa Mataifa ya kutaka kuongezewa eneo la Ukanda wa Bahari Kuu. *(Makofi)*

Lakini pia Baraza lako Tukufu lilipokea ripoti mbili, moja ikiwa ya Tume ya Haki za Binaadamu kwa mwaka 2007/2008 na Ripoti ya Hitilafu ya Vyombo vya Usafiri Baharini za hivi karibuni. Natumai ripoti hizo zilikonga nyoyo za Waheshimiwa

Wawakilishi.

Mhe. Spika, Wajumbe wa Baraza pia walipata Semina kuhusu Mageuzi ya Teknolojia kutoka *Analogy* kwenda *Digital*, Semina kuhusu Soko la Pamoja la Afrika Mashariki na Semina kuhusu Bajeti inayozingatia *Program* (*Program Based Budget*). Semina zote hizi ziliwapa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu uelewa mpana zaidi wa mambo hayo.
Mhe. Spika, katika kuujadili Mswada wa Sheria ya Kuweka Mafao ya Viongozi Pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo, Serikali imepokea kwa moyo mkunjufu maoni ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kuhusu Mswaada huo. Maoni yalikuwa mengi na mazuri, kwa sababu maoni hayo yanataka kufanyiwa kazi kwa umakini mkubwa. Serikali imeamua kuuahirisha Mswada huo ili maoni hayo yaweze kuzingatiwa zaidi. *(Makofi)*

Mswada huo utarejeshwa tena katika kikao kijacho cha mwezi wa Machi cha Baraza lako kwa majumuisho. Kwa niaba ya serikali, nachukua fursa hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Wajumbe wote kwa namna walivyochangia Mswaada huu. *(Makofi)*

Nia ya serikali si kuongeza mafao kwa Viongozi wa Kisiasa bali ni kuwajengea heshima viongozi wetu wakati wanapostaafu baada ya kazi kubwa waliyoifanya katika utumishi wao na kwa kufanya hivyo tutakuwa tunalijengea heshima kubwa Taifa letu na Viongozi wake. Hivyo, naamini kuwa utaporejeshwa tena kwa majumuisho, marekebisho yataturidhisha sote na tutakuwa na sheria nzuri yenye maslahi kwa nchi yetu na watu wake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuhusu Mswaada wa Kuanzishwa Mamlaka ya Rushwa, serikali imepokea ushauri, maoni na mapendekezo ya Wajumbe wa Baraza lako tukufu. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kuwa serikali itakuwa makini sana katika kusimamia chombo hiki. Kwani kama tunavyoelewa kuwa rushwa

ni adui wa haki na ni adui mkubwa sana wa maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Suala la rushwa linamgusa kila mmoja wetu wakati wa kutafuta haki zetu. Kuundwa kwa Mamlaka hii ni hatua moja ya kupambana na rushwa, lakini jambo kubwa zaidi linalohitajika ni kuwa kila mmoja wetu kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya rushwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika hotuba yangu ya kufunga Mkutano wa Watano wa Baraza lako Tukufu nilizungumzia tukio la kuzama kwa meli ya *M.V. Spice Islander I* katika eneo la Nungwi iliyokuwa ikitokea Unguja kuelekea Kisiwani Pemba tarehe 10 Septemba, 2011 majira ya saa 9 usiku. Tukio hili kama tunavyoelewa lilileta maafa makubwa katika nchi yetu na ni msiba uliotugusa sote.

Tunazidi kumuomba Mwenyezi Mungu awapumzishe mahala pema peponi wenzetu wote waliotangulia mbele ya haki katika ajali hiyo na Mungu azidi kuwapa subira wale wote waliopoteza ndugu, rafiki na jamaa zao. Kwa walionusurika Mungu azidi kuwapa afya njema, ili warejee katika hali zao za kawaida za kimaisha.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza mara nyingi, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliunda Tume yenye Wajumbe 10 ikiongozwa na Jaji Abdulhakim Ameir Issa kama Mwenyekiti wa Tume hiyo, iliyopewa kazi ya kuchunguza sababu na chanzo cha ajali ya meli ya *M.V. Spice Islander I.*

Mhe. Spika, sasa naomba kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa Tume hiyo imemaliza kazi yake na kuwasilisha ripoti yake kwa Mhe. Rais tarehe 5 Disemba, 2011. Kama Mhe. Rais wetu alivyoahidi Ripoti ya Tume hiyo imetolewa hadharani na wananchi kuelezwa bayana yaliyobainika katika uchunguzi wa Tume hiyo.

Katika ripoti yake Tume ilitoa mapendekezo yake, ambayo serikali imeyachukua na imeshaanza kuyafanyia kazi na hatua kuchukuliwa kwa wale wote waliohusika ama kwa moja kwa moja au si kwa moja kwa moja kama ilivyopendekezwa.

Mhe. Spika, katika mapendekezo yake Tume imetoa mambo saba ya kufanyiwa kazi. Mambo hayo ni:-

(a) Hatua za kisheria na kinidhamu kwa wahusika wa moja kwa moja na ajali hiyo;

(b) Hatua za kinidhamu kwa wahusika wasiokuwa wa moja kwa moja;

(c) Mapendekezo ya hatua za kisheria kwa kampuni husika;

(d) Mapendekezo ya namna ya kuimarisha usafiri bandarini;

(e) Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria;

(f) Mapendekezo ya kuimarisha uokozi; na

(g) Mapendekezo ya ulipaji fidia;

Mhe. Spika, naomba kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba, serikali tayari imeanza kuyafanyia kazi mapendekezo hayo na narudia kusema kwamba serikali haitokuwa na muhali juu ya utekelezaji wa mapendekezo hayo. Hivi sasa tayari baadhi ya wahusika wameshapelekwa katika Vyombo vya Sheria na wengine kuchukuliwa hatua za kinidhamu kama ilivyopendekezwa. *(Makofi)*

Aidha, ningependa kulieleza Baraza lako Tukufu kwamba ripoti

hii itawekwa katika mtandao ili kila mtu aisome, na pia itawekwa kwenye Maktaba Kuu ya Taifa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kuipongeza kwa dhati Tume hiyo kwa kazi nzuri waliyoifanya kukamilisha ripoti hiyo, ambapo uchunguzi wake ulifanywa kwa umakini mkubwa. Kwa niaba ya serikali ninawashukuru sana Wajumbe wote wa Tume.

Mhe. Spika, napenda kuwajuilisha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu pamoja na wananchi wote kwa ujumla kwamba, baada ya kupokea taarifa ya Tume na kuwa na orodha kamili ya waliopatwa na ajali hiyo hivi karibuni serikali itazigawa fedha za misaada zilizochangwa na wananchi na wahisani mbali mbali kwa wahanga wa ajali hiyo. *(Makofi)*

Hadi tarehe 26 Januari, 2012 jumla ya fedha zilizopatikana ni shilingi 1,231,203,861.00/= na fedha zote hizo zipo katika Akaunti Maalum ya Maafa iliyopo Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*) na hakuna fedha hata moja iliyotumika hadi sasa kwa matumizi mengine. *(Makofi)*

Gharama zote zilizojitokeza katika operesheni ya maafa haya zilitolewa na Serikali. Nachukua fursa hii kuwashukuru wananchi wote kwa uvumilivu na utulivu wao wakati wakisubiri Tume kukamilisha kazi zake. Aidha, nawashukuru wote waliotoa misaada mbali mbali ya hali na mali katika operesheni nzima ya maafa hayo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tarehe 12 Januari, 2012 nchi yetu ilitimiza miaka 48 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Hili ni jambo la kujivunia kwetu na kwa vizazi vyetu. Kama tunavyoelewa, sherehe hizo zilitanguliwa na mambo kadhaa ikiwemo uzinduzi wa miradi 24 ya maendeleo.

Katika kilele cha maadhimisho ya sherehe hizo Rais wa Zanzibar

na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein alitoa hotuba ambayo iliainisha maeneo mbali mbali ya maendeleo katika nchi yetu, hali ya utulivu wa kisiasa inayotokana na mfumo wetu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa na kuelezea juu ya changamoto zinazoikabili nchi yetu hivi sasa.

Mhe. Spika, nisingependa kurejea kilichoelezwa katika hotuba iliyotolewa na Mhe. Rais, isipokuwa naomba kutoa wito kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, Viongozi wote wa Serikali na wananchi wote wa Zanzibar kuendeleza umoja na mshikamano wetu na kufanya kazi kwa bidii zaidi katika kuiletea nchi yetu maendeleo.

Kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, natoa shukrani kwa Wajumbe wa Baraza, Viongozi wote wa Serikali na Vyama vya Siasa na Mashirika ya Serikali na Sekta Binafsi na wananchi wote wa Zanzibar na Tanzania kwa kufanikisha sherehe zetu hizi kwa mafanikio makubwa sana. Ni imani yangu tutaendelea kushirikiana zaidi katika kufanikisha sherehe zijazo.

Naomba tukumbuke kwamba miaka miwili kutoka sasa tutasherehekea kutimiza miaka 50 (Nusu Karne) ya Mapinduzi yetu. Maandalizi ya sherehe hizo yanahitaji kuanza sasa na kila mmoja wetu mchango wake unahitajika.

Mhe. Spika, Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Mawasiliano (*ITU*) limefanya maamuzi kwa Mataifa duniani kufanya mageuzi ya Televisheni kutoka mfumo wa utangazaji wa *Analogy* kwenda *Digital* ifikapo tarehe 31 Disemba, 2012.

Katika kuhakikisha kwamba Zanzibar inakwenda sambamba na mabadiliko hayo, serikali imeanza kuchukua hatua mbali mbali, ili kuhakikisha kwamba ifikapo tarehe 31 Disemba, 2012 iwe tayari tumeshahamisha matangazo kutoka *Analogy* kwenda *Digital*. Miongoni mwa hatua zinazochukuliwa ni kuwasiliana na

makampuni mbali mbali duniani, kwa ajili ya kupatikana vifaa vinavyohitajika na kutafuta fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa hivyo.

Aidha, napenda kutoa wito kwa wananchi kuanza kuchukua hadhari juu ya ununuzi wa seti za televisheni ambazo hazina mfumo wa *Digital*. Naagiza chombo cha Tume ya Utangazaji watoe elimu zaidi kwa wananchi kuepuka kununua seti za televisheni ambazo ni za mfumo wa *Analogy* kwani hazitaweza kutumika tena itakapofika Disemba 2012. Ili kuepuka usumbufu, naomba waanze kufikiria suala hilo kwa makini na kutoa maamuzi sahihi wakati muda bado upo. Nawasihi sana wale wenzetu wanaoingiza televisheni zilizotumika waache kufanya hivyo kwa sasa kwani kutaifanya nchi yetu kuwa dampo, na hivyo kuharibu mazingira.

Mhe. Spika, nchi yetu hivi sasa imo katika maandalizi ya kufanyika kwa Sensa ya mwaka 2012. Sensa hiyo inafuatia ile iliyofanyika 2002 na imepangwa kufanyika tarehe 26 Agosti, 2012. Sensa hii itakuwa ni ya tano kufanyika tokea kupata Uhuru. Sensa zilizokwisha fanyika kabla zilifanyika mwaka 1967, 1978, 1988 na 2002.

Sensa ya Watu na Makaazi ni chanzo muhimu cha takwimu, ambazo hutumika katika kutayarisha Sera za kijamii na kiuchumi na hutumika kutathmini ubora wa hali ya maisha ya watu kwa ujumla. Takwimu zitakazokusanywa katika Sensa ya mwaka 2012 zitatumika kutathmini programu mbali mbali za maendeleo kama vile MKUZA, Malengo ya Milenia ifikapo 2015 na kutumika na wadau mbali mbali.

Naomba kuchukua nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wote kushiriki kikamilifu katika kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa Sensa na kuwataka kushiriki kwa kutoa majibu sahihi wakati ukifika. Ninawasihi wananchi wasiliogope jambo

hili wala kulikimbia, kwani ni jambo muhimu sana litakalosaidia serikali yetu kupanga vizuri mipango yake ya maendeleo.

Mhe. Spika, nalipongeza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupitisha Mswada wa Sheria ya Kuweka Utaratibu wa Kuratibu Maoni ya Wananchi kuhusu Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilishirikishwa kikamilifu katika maandalizi yote ya Mswada huo. Tunaishukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mashirikiano makubwa walioyaonesha kwa Zanzibar katika mchakato mzima wa maandalizi ya Mswaada huu. Naomba niwasihi wananchi wenzangu wote, tushiriki kikamilifu katika kutoa maoni yetu wakati utakapowadia. *(Makofi)*

Hii ni fursa pekee ya kutoa kila tunachohisi kinafaa kwa manufaa ya nchi yetu na watu wake. Tutoe maoni yetu bila ya woga na hakutokuwa na sababu ya kuwa na woga kwani kutoa maoni ni haki ya kila mwananchi Kikatiba. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ifikapo tarehe 12 Februari, 2012 nchi yetu itakabiliwa na zoezi la uchaguzi mdogo wa Jimbo la Uzini katika Wilaya ya Kati, Unguja. Uchaguzi huo utafanyika kufuatia kifo cha aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo hilo marehemu Mussa Khamis Silima. Maandalizi ya uchaguzi huo yameanza kwa Vyama vya Siasa kusimamisha wagombea wao. Wito wangu kwa wananchi wa Jimbo la Uzini na wanachama wa vyama vya siasa vitakavyoshiriki katika uchaguzi huo kutumia haki yao ya kikatiba kupiga kura kwa amani, ili tuweze kuendeleza amani na utulivu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuendelea kutekeleza azma yake ya kuleta mapinduzi ya kilimo katika nchi yetu, inaendelea kuchukua hatua mbali mbali zitakazosaidia kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara na hivyo kusaidia kujenga uchumi wa nchi yetu na kuwaongezea

mapato wakulima.

Hivi karibuni serikali kwa makusudi imetoa ruzuku kwa wakulima, hasa kwa wakulima wa zao la mpunga. Ruzuku hii imetolewa kwa ajili ya kuwapunguzia mzigo mkubwa wa bei wakulima katika pembejeo za kilimo. Katika hatua hiyo, serikali imepunguza gharama za uchimbaji na uburugaji kwa matrekta kwa asilimia 73.
Hivi sasa wakulima wanachangia gharama za uchimbaji na uburugaji kwa kutoa shilingi 32,000/= kwa ekari moja. Bei halisi ilipaswa kuwa shilingi 120,000/=. Vile vile, bei ya mbegu bora ya mpunga nayo imepunguzwa ambapo mkulima anauziwa mbegu hizo kwa bei ya shilingi 200/= kwa kilo badala ya shilingi 1,500/=, ambayo ndio bei iliyopaswa kuuzwa mbegu hizo. Hii ni fidia ya asilimia 87. *(Makofi)*

Kwa upande wa mbolea pia bei imepunguzwa kutoka shilingi 60,000/= kwa polo ya kilo 50, na kuuzwa kwa bei ya shilingi 10,000/= kwa mfuko wa Kilo 50. Hili ni punguzo la asilimia 83. Aidha, bei ya kuulia magugu wanayotozwa wakulima hivi sasa ni shilingi 6,000/= kwa lita moja badala ya shilingi 12,500/= iliyopaswa kulipwa, ikiwa ni punguzo la asilimia 52. Bei hizi za ruzuku tayari zimeanza kutumika rasmi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, serikali ikiwa na dhamira ya kweli ya kuwakomboa wakulima na kulirejeshea hadhi yake zao la karafuu ilichukua hatua za makusudi za kupandisha bei ya karafuu kutoka Shilingi 3,500/ kwa kilo hadi kufikia Shilingi 15,000/ kwa kilo. Bei hii mpya ya kununulia karafuu kutoka kwa wakulima kupitia Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) ilitangazwa na kuanza kutumika tokea tarehe 3 Julai, 2011.

Wapo watu waliothubutu kuwadanganya wananchi kuwa kwa bei hiyo serikali isingeweza kununua karafuu zote kutoka kwa wakulima. Sasa imedhihirika kwamba maneno hayo ya watu

wachache wasioitakia nchi yetu maendeleo si ya kweli kwa vile hadi sasa serikali inaendelea kununua karafuu bila ya kutetereka.

Naomba kurejea maneno ya Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein kwamba serikali haitashusha bei ya zao hilo hata kama bei katika soko la dunia itashuka. Na kwa pale bei ya karafuu ikipanda na serikali nayo itawaongezea bei wakulima. Katika kuthibitisha kauli ya Mhe. Rais, hata bei ya karafuu iliposhuka katika soko la dunia katika msimu huu kutoka Dola za Kimarekani 16,000 kwa tani hadi kufikia kiwango cha bei ya Dola kati ya 10,000 na 12,000 kwa tani, bado serikali imeendelea kununua kutoka kwa wakulima kwa bei ile ile ya Shilingi 15,000 kwa kilo bila ya kuwakopa.

Mhe. Spika, napenda kulijuilisha Baraza lako Tukufu kwamba hadi kufikia tarehe 25 Januari, 2012, jumla ya tani 4,479 za karafuu zilikuwa tayari zimeshanunuliwa na ZSTC na hivyo wakulima kujipatia jumla ya Shilingi Bilioni 66.95. Napenda kutoa wito kwa wakulima wa karafuu na wananchi wote kujenga utamaduni wa kuhifadhi fedha zao Benki. Hii inasaidia kuweka usalama wa fedha zao pamoja na kusaidia harakati za kiuchumi katika nchi yetu.

Mhe. Spika, serikali itaendelea na jitihada zake za kuwasaidia wakulima na kuimarisha Sekta ya Kilimo ili kuwa na kilimo chenye tija na kuchangia kwa kiasi kikubwa pato la Taifa na hivyo kuchangia katika kupunguza umasikini.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kutoa kipaumbele kwa Sekta ya Utalii. Hii inatokana na sekta hii kuwa na mchango mkubwa katika uchumi wa nchi yetu. takwimu zinaonesha kwamba katika mwaka wa 2010/2011, Zanzibar imepokea jumla ya watalii 175,670 kutoka nje ya nchi. Idadi hii ni kiwango kikubwa ikilinganishwa na idadi ya watalii 132,836 walioingia nchini mwaka 2010, hizi ni habari njema sana kwetu.

Hivyo natoa wito kwa wananchi wote wa Zanzibar kuendelea kuunga mkono hatua za serikali katika kuikuza Sekta ya Utalii. Aidha, natoa wito kwa Taasisi husika na utalii kuendelea na kazi nzuri wanayoifanya ya kutafuta masoko mapya hasa ya nchi kama China, Uturuki, Japan na Urusi, ambao wananchi wake tayari wameanza kutembelea nchi yetu kama watalii.

Wakati tukijitahidi kuongeza idadi ya watalii, naomba sana tuendeleze utamaduni wetu wa kuwaheshimu wageni wetu hawa. Tusiwabughudhi wala kuwakera kera wakati wakifanya shughuli zao za kitalii kama vile kuongelea katika bahari yetu nzuri au katika matembezi yao. Nawasihi sana Mapapasi waache tabia zao za kuwakera kera watalii wetu. Lengo la serikali yetu ni kuongeza watalii mpaka kufikia mia mbili na hamsini elfu (250,000) ifikapo 2015

Mhe. Spika, sote ni mashahidi wa kiasi gani nchi yetu inavyoendelea kupiga hatua katika kazi ya ujenzi wa barabara. Katika kipindi kifupi kijacho naamini tutaweza kuunganisha miji na vijiji vingi kutokana na kuwa na barabara bora za lami. Hivi karibuni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amezizindua barabara sita mpya katika Kisiwa cha Pemba. Kumalizika kwa barabara hizi kutafungua milango ya shughuli za uwekezaji na kuimarisha biashara na upatikanaji wa masoko kwa urahisi kwa bidhaa za wananchi. Barabara zilizozinduliwa kwa upande wa Kisiwa cha Pemba ni:-

i) Mtambile – Mwambe (km 9.4)

ii) Mizingani – Wambaa (km 9.7)

iii) Mtambile – Kangani (km 6.2)

iv) Kenya – Chambani (km 3.2)

v) Chanjamjawiri – Tundaua (km 11)

vi) Chanjaani – Pujini (km 5)

Kwa upande wa Unguja, barabara ya Amani – Dunga yenye urefu wa kilomita 12.7 ikiwa na daraja jipya la Mwera tayari imekamilika na kuzinduliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika maadhimisho ya kutimiza miaka 48 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, barabara ya Mfenesini – Bumbwini yenye urefu wa Kilomita 13.2 matengenezo yake yanaendelea vizuri na hivi karibuni itakamilika.

Mhe. Spika, nawapongeza kwa dhati viongozi na watendaji wote wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kazi zao nzuri na nawataka waendelee na juhudi zao hizo.

Mhe. Spika, sambamba na lengo hilo la kuimarisha miundombinu ya mawasiliano nchini, serikali inaendelea kuchukua hatua za kuimarisha jengo la abiria la Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume. Sote tumeona umuhimu wa kuweka uwanja wetu wa ndege katika hali bora kwa viwango vinavyokubalika kimataifa. Suala hilo linatakiwa kwenda sambamba na ukuaji wa shughuli za uwekezaji katika sekta muhimu za biashara na utalii. Lengo ni kuhakikisha kuwa tutakuwa na jengo zuri lenye hadhi na uwezo wa kutoa huduma kwa wasafiri wasiopungua 1,600 kwa wakati mmoja. Hili ni jambo jema kwa nchi yetu na hatuna budi sote kuliunga mkono, na hasa wale wananchi wenzetu wanaoishi karibu na maeneo ya Uwanja wa Ndege.

Mhe. Spika, katika azma ya uboreshaji wa kiwanja cha ndege sambamba na haja ya kuhakikisha kuwa kiwanja kinakidhi mahitaji, serikali inaendela kuchukua hatua za kupata mkandarasi ambae atafanya kazi ya kupanua njia za ndege *(Tax-Way)* na maeneo ya maegesho ya ndege (*Apron*). Kukamilika kwa mradi huo ambao utagharimu Dola za Kimarekani 54 milioni utasaidia sana kupunguza tatizo la ufinyu wa nafasi kwa ndege zinazoingia

na kutoka uwanjani hapo. Jambo hili litasaidia sana kuvutia Mashirika mengi zaidi ya ndege kutumia uwanja huo na kuongeza pato letu la Taifa.

Mhe. Spika, Zanzibar ikiwa ni sehemu ya dunia inakabiliwa na tatizo la athari za mabadiliko ya tabia nchi. Aidha, nchi yetu inakabiliwa na changamoto mbali mbali za kimazingira zinazotokana na ukataji ovyo wa misitu na upotevu wa bioanuwai za nchi kavu na baharini, utupaji ovyo wa taka na maji machafu na uchukuaji usioridhisha wa maliasili zisizorejesheka. Hali hii ikiachiwa kuendelea nchi yetu itakumbwa na tatizo kubwa la athari za kimazingira. Naomba kuchukua fursa hii kuzidi kuhamasisha jamii kuchukua hatua muafaka za kupunguza athari zinazotokana na mabadiliko ya Tabia Nchi.

Aidha, nawaasa wananchi pamoja na kuwahimiza wataalamu wetu kuendelea kuchukua juhudi zaidi kutafuta njia mbadala za kuweza kudhibiti uharibifu wa mazingira yetu. Aidha, mazingira ya nchi yetu yanaharibiwa na vitendo vya uchimbaji wa mchanga. Vitendo hivi vikiachiliwa kuendelea, nchi yetu itakuwa ya mashimo matupu, ambapo mashimo mengine yakijaa maji yanahatarisha maisha ya watoto wetu.

Mhe. Spika, dawa za kulevya bado ni tishio kwa vijana wetu hapa nchini. Ingawa juhudi kubwa zinaendelea kuchukuliwa na serikali kupitia Taasisi za Kiserikali na zisizo za Kiserikali katika kukabiliana na athari za tabia hiyo ya utumiaji wa madawa ya kulevya, bado kazi kubwa inahitajika kufanywa kuweza kuwanusuru vijana wetu dhidi ya madawa hayo thakili.

Mhe. Spika, nawasihi wale wote wanaojihusisha na madawa ya kulevya kwa namna yoyote ile kuacha tabia hiyo mara moja ili kusaidia nchi yetu kuondokana na matatizo yanayosababishwa na madawa hayo. Taasisi zinazohusika na udhibiti wa madawa ya kulevya hawana budi kuchukua hatua na mikakati madhubuti ya

kuwachukulia hatua za kisheria wale wote wanaojihusisha na madawa hayo ya kulevya. Mhe. Spika, pamoja na hatua hiyo, serikali inaendelea kushirikiana na Washirika wa Maendeleo katika kutoa mafunzo ya kuwasaidia walioathirika na madawa hayo thakili kuweza kuondokana na tatizo hilo.
Mhe. Spika, migogoro ya ardhi hasa maeneo yaliyopakana na fukwe bado ni tatizo sugu linaloisumbua serikali na nchi yetu kwa jumla. Hali hii ikiachiwa kuendelea tutaitumbukiza nchi yetu katika janga la uhasama miongoni mwa wananchi na hatimaye wananchi dhidi ya Viongozi na serikali yao. Migogoro hii ya ardhi ipo Kaskazini na Kusini Unguja. Kwa upande wa Kaskazini kuna migogoro ya ardhi Pwani Mchangani, Kiwengwa, Nungwi na kwa upande wa Kusini Unguja migogoro hiyo ipo Mtende na maeneo mengine.

Sababu kubwa inayochochea migogoro ya ardhi ni kupanda kwa thamani ya ardhi iliyopakana na fukwe. Leo hii dau linalotolewa kwa kipande cha ardhi ambacho zamani kiliuzwa kwa shilingi laki chache tu leo hii kinauzwa kwa milioni nyingi za fedha. Mamilioni haya ya fedha yanayotolewa mara nyingi na wawekezaji katika sekta ya utalii, yamejenga tamaa miongoni mwa wananchi wakorofi wakishirikiana na Viongozi walafi kuuza ardhi bila ya kufuata utaratibu wa kisheria uliowekwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sisi Viongozi wa ngazi mbali mbali kwa upande mwingine tunahusika na migogoro hii. Masheha na Madiwani kwa mfano wanachangia kwa asilimia kubwa ya migogoro ya ardhi katika maeneo niliyoyataja. Mhe. Spika, kiongozi kazi yake kubwa ni kuonyesha njia ya matumaini kwa wananchi anaowaongoza. Kiongozi anayeonyesha njia inayoelekea kwenye uporaji wa ardhi hatufai.

Mhe. Spika, kwa wale Wawakilishi wanaotoka katika maeneo yanayokabiliwa na migogoro ya ardhi tuondokeni hapa leo hii na dhamira ya kuwa suluhisho. Tusaidie kuelimisha wananchi wetu

kuachana na tamaa ya kuuza ardhi kiholela. Tuwaelimishe pia Masheha na Madiwani wetu kuachana na tabia ya kitapeli ya kuuza ardhi. Serikali itachukua hatua mbali mbali kuirekebisha hali hii ili iweze kupungua na kumalizika kabisa. (*Makofi*)
Mhe. Spika, kwa kumalizia napenda kuchukua nafasi hii kwa mara nyengine kukushukuru kwa dhati kabisa wewe binafsi, kwa kuliendesha Baraza letu kwa mafaniko makubwa. Lakini pia napenda kumshukuru Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza ambao wamekuwa wakikusaidia mara kwa mara.

Kwa mara nyengine tena nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa mashirikiano mazuri katika kikao hiki na hadi kufika leo hii tunamaliza kwa mafanikio. Aidha, napenda kuwashukuru sana waandishi wetu wa habari kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuwawezesha wananchi kuyaona mambo yote yaliyokuwa yanatokea ndani ya Baraza, waliyoyapenda na wasiyoyapenda, yote waliyaona. Nachukua fursa hii kuwatakia Wajumbe wote kurudi katika sehemu zao za kazi kwa salama na amani na pia turejee Majimboni mwetu kwenda kuendelea kushirikiana na wananchi wetu katika kuwaletea maendeleo na kuiletea maendeleo nchi yetu.

Mwisho nawatakia heri na baraka za mwaka mpya wa 2012. Ni matumaini yangu kwamba tukirudi hapa kwa kikao kijacho, tutarudi kama watu wamoja, wenye upendo na mshikamano.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kutoa hoja ya kuliahirisha Baraza lako Tukufu hadi Jumatano, tarehe 28 Machi, 2012 saa 3 asubuhi. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa Iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

Hoja ya Kuakhirisha Mkutano wa Sita wa Baraza la Wawakilishi

MATANGAZO

Mhe. Spika: Mhe. Makamo wa Pili wa Rais nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa hotuba nzuri sana, ambayo makofi mengi yanayopigwa bila ya shaka imewagusa ndipo Waheshimiwa Wajumbe.
Huo ndio muelekeo ambao sisi viongozi tupaswa tuwe. Nakushukuru sana Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuwahoji nataka nitoe matangazo mawili madogo.

1) Siku ya tarehe 30 tutakuwa na Semina pale *Zanzibar Beach Resourt* Semina hiyo inatuhusu ule Mswada wa siku nyingi ambao tumekuwa tunaudai tunaombwa sote tuhudhurie semina hii. Ili kusiwe na suali tunaambiwa mambo siyo mabaya ni mambo mazuri.

2) Waheshimiwa Wajumbe, kutoka Chama cha CUF wanaombwa mara ya kumaliza shughuli yetu hapa wakutane hapo juu kwenye ukumbi wa juu, kuna mazungumzo yanataka kutolewa kwao. Naomba na wao pia wahudhurie mkutano huo.

Waheshimiwa Wajumbe, basi nakushukuruni na sasa naomba niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ya Kuakhirisha Mkutano huu hadi tarehe 28/3/2012 Saa 3:00 za asubuhi, wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

Sasa nirudie tena kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa kumaliza shughuli zetu salama. Tunaondoka wamoja, tunarudi wamoja kama Mhe. Makamo wa Pili alivyosema. Na sasa naakhirisha Kikao hichi hadi siku ya Jumatano tarehe 28/3/2012, saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 05:15 asubuhi Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 28 Machi 2012 Saa 3:00 za asubuhi)

WIMBO WA TAIFA